***HOTUBA YA MHE KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MP), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANIO WA TANZANIA ITAKAYOSOMWA KATIKA MAHAFALI YA PROGRAMU ZA UONGOZI ZITOLEWAZO NA TAASISI YA UONGOZI, UKUMBI WA MLIMANI CITY, DAR ES SALAAM TAREHE 5 MEI 2023***

- **Mhe. George Simbachawene**, Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora,
- **Eng. Zena Ahmed Said**, Katibu Mkuu Kiongozi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar,
- **Mhe. Wamkele Mene**, Katibu Mtendaji, Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara Afrika (African Continental Free Trade Area-AfCFTA),
- **Ndugu Mululi Majula Mahendeka**, Katibu Mkuu Ikulu
- **Balozi. Ombeni Sefue**, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Taasisi ya UONGOZI,
- Mabalozi na Maafisa wa Balozi mbalimbali mliopo,
- **Ndugu Kadari Singo**, Afisa Mtendaji Mkuu Taasisi ya UONGOZI
- **Prof. Pekka Mattila**, Muwezeshaji na Muwakilishi Chuo Kikuu cha Aalto -Finalnd,
- Wakuu wa Taasisi na Wadau mbalimbali mliohudhuria
- Wakufunzi, Wahitimu na Washiriki wapya wa Mafunzo ya Uongozi,

- Ndg. Wageni waalikwa,
- Waandishi wa habari,
- Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyetujalia uhai na kutuwezesha kuiona siku ya leo. Napenda pia nitumie fursa hii kumshukuru Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kunipa nafasi hii ya pekee kumwakilisha yeye ambae alialikwa kuwa mgeni rasmi katika mahafali ya Programu za mafunzo ya uongozi. Asante sana Mhe Rais. Hotuba hii ni ya Mhe Rais na nitaisoma kwa niaba yake na pale nitakapoona inafaa nitaongeza maneno machache.

Aidha, nikushukuru sana Mhe Waziri kwa kuendelea kusimamia na kuhimiza umuhimu wa mafunzo na semina elekezi kwa viongozi na watumishi wa umma. Naomba muendelee kujipanga ili kuhakikisha mafunzo ya uongozi na semina elekezi zinatolewa kwa viongozi na watumishi wote wa serikali na mihimili mingine.

Kwa njia ya pekee, nipende kumshukuru **Mhe. Wamkele Mene**, Katibu Mtendaji, Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara Afrika (African Continental Free Trade Area-AfCFTA), kwa safari ndefu toka Accra, Ghana kwa kuona umuhimu wa kuwajenga viogozi na kuwa sehemu ya uwasilishaji na kuelezea uzoefu wake wa kiuongozi barani Africa. Karibu sana Mhe. Wamkele Mene.

Aidha naipongeza Taasisi ya UONGOZI kwa kuendelea kutimiza jukumu kubwa la kutoa mafunzo kwa viongozi wa ngazi mbalimbali hapa nchini ili kuiwezesha serikali kufikia malengo.

Kuandaa na kuendeleza viongozi si jambo la hiari bali ni la lazima. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema ili tuendelee tunahitaji mambo manne: Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora. Ni dhahiri kuwa uongozi bora ni nguzo iliyoshikilia haya mambo mengine matatu. Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, kuna jumla ya Watu 61.7 milioni, ambapo wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka ni 3.2. Ingawa Nchi yetu imebarikiwa ardhi yenye rutuba na rasilimali za asili nyingi lakini mtakubaliana nami kuwa bila uongozi bora ni ngumu sana kupata maendeleo tunayoyakusudia.

Hivyo basi, nijukumu letu sote kama taifa kuhakikisha tunakuwa na uongozi bora utakao simamia haya mambo mengine matatu ili kufikia maendeleo endelevu na kuimarisha ustawi wa Taifa. Hapa naomba Taasisi ya UONGOZI kutambua inamchango inachagia kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 inayotekelezwa na mpango wa maendeleo wa miaka mitano mitano ambapo kwa sasa tupo katika mpango wa tatu na wa mwisho wa utekelezaji wa Dira hii ambao umeweka bayana umuhimu wa kujenga mazingira bora ya uongozi, utawala na uwajibikaji.

**Ndugu Wahitimu**

Kwa dhati kabisa napenda kuwapongeza kwa kumaliza mafunzo haya muhimu ya uongozi. Ni matumaini yangu mafunzo mliyoyapata yatawafanya kuwa chachu ya mabadiliko katika maeneo yenu ya kazi, na

mtakwenda kukuza na kuimarisha utawala bora wenye kufuata haki, sheria, kanuni, miongozo na taratibu tulizojiwekea, kuimarisha uwajibikaji, kuongeza ubunifu na kuimarisha utendaji wa kazi ili kulisaidia taifa kufikia malengo tuliyojiwekea.

**Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,**
Suala la usawa wa kijinsia ni muhimu sana kwenye kufikia maendeleo endelevu. Bado kumekua na changamoto ya ufinyu wa Wanawake kwenye nafasi za juu za uongozi. Nimefarijika sana, kufahamu kuna Programu maalum ya mafunzo ya Uongozi kwa viongozi Wanawake; maana haitoshi kuwachagua, kuwateua na kuwapa nyadhifa wanawake watumishi kama hawajaelimika vya kutosha. Juhudi za kukwamua wanawake lazima ziendane na juhudi za kulea na kukuza vipaji vyao vya uongozi ili wanapopatiwa nafasi waweze kuonyesha kwa vitendo namna gani Wanawake wanaweza kubadili Jamii na kuleta maendeleo.

Nawaasa Viongozi Wanawake mnaohitimu mafunzo haya mkaonyeshe kwa vitendo kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, kufanya maamuzi kwa kujiamini; na zaidi mkashirikane na akina baba katika utendaji.

Wanawake, kuwezeshwa kielimu na kiuchumi isiwe sababu ya kuibua jeuri na majivuno mara mpandapo vyeo au kuongezeka kwa pato lenu, mkifanya hivi mtaharibu juhudi za Serikali. Lengo letu ni kuwa na Viongozi wanawake watakaokuwa chachu ya kuleta maendeleo kuanzia ngazi ya familia mpaka taifa. Tunaamini Wanawake walioelimika ni chachu ya maendeleo yenye tija kwa jamii nzima.

Shime sasa viongozi wanawake mnaohitimu, msiende kukaa kusubiri mpaka mpandishwe vyeo ama kuteuliwa nendeni mkathubutu kuingia kwenye michakato ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, si Ubunge tu ila na nyingine zinazohitaji ushindani; uwezo mnao na nguvu mnazo na nyenzo mmepata. **HONGERENI VIONGOZI WOTE WANAWAKE, NYENZO MNAZO SASA KAZI IENDELEE, MKAUPIGE MWINGI TAIFA LISONGE MBELE.**

**Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,**

Ili kufikia malengo makuu ya kiuchumi ushirikiano kati ya Sekta Binafsi na sekta ya umma (*Public Private Partnership)* ni muhimu katika kuchagiza uchumi kupitia kuanzisha na kukuza uwekezaji na biashara. Hivyo kuna umuhimu wa kuwajenga viongozi wa sekta zote za umma na binafsi. Napenda kusisitiza umuhimu wa Taasisi ya UONGOZI kuangalia kwa namna gani itashawishi viongozi wa Sekta binafsi kupatiwa mafunzo haya ya uongozi kwa mfumo wa kuchangia gharama. Natambua kuwa mmeshaanza ndiyo maana leo tuna wahitimu kutoka sekta binafsi ambao wamenufaika na mafunzo haya. Hivyo naomba kutoa rai kwa viongozi wa mashirika binafsi kuitumia Taasisi ya UONGOZI ili kuwanoa viongozi wao maana wote tunajenga nyumba moja na kama nchi tunahitaji viongozi bora katika sekta zote ili kulipatia Taifa mendeleo tuliyokusudia.

**Ndugu Wahitimu na Wageni Waalikwa,**

Suala la kuandaa viongozi na kuwajengea uwezo ni endelevu na linahitaji utaalamu na wanataaluma wenye ueledi na rasilimali za kutosha kulifanikisha kwa viwango vinavyostahili. Nasisitiza Taasisi ya UONGOZI iendelee kuwatumia viongozi wakuu wastaafu pamoja na wakufunzi

wengine mahiri wa ndani maana wana uzoefu wa kutosha na uwepo wao ni hazina kwetu, tuwatumie.

**Ndugu Wahitimu,**

Ndugu wahitimu wa leo, na wengine mliokwisha wahi pata mafunzo haya, Serikali inawategemea sana katika kufanikisha maboresho makubwa na kuleta tija katika utoaji huduma kwa jamii.

Suala la uratibu wa shughuli za Serikali na miradi ya maendeleo umekuwa na changamoto nyingi zinazoathiri ufanisi. Ninatoa rai kwenu, huko muendako mkasaidie kutafuta njia bora zaidi za kuratibu utekelezakaji kwa kutumia rasimali chache na kupelekea matokeo makubwa na chanya kwa miradi ya maendeleo.

Ndugu Wahitimu, mmefundishwa umuhimu wa ubunifu na uvumbuzi, uthubutu, namna ya kuongoza watu na kusimamia rasilimali, kushirikiana, kuheshimiana na kutenda haki; mmefundishwa maadili na utawala bora pamoja na athari za rushwa katika kutekeleza majukumu yenu kama watumishi; yote haya yatoshe kusema sasa tunataka kuona utumishi bora wenye misingi imara na dhabiti ya kiuongozi. Hatutegemei kuona mnaowaongoza au nyie wenyewe mkijihusisha na masuala ya rushwa, ubadhilifu na vitendo vya unyanyasaji ndani na nje ya kazi. **NENDENI MKATENDE HAKI, MKAONDOSHE KERO KWA WANANCHI KWA KUBORESHA HUDUMA.**

**Ndugu washiriki mnaonza mafunzo,**

Ni ukweli usiopingika kuwa miongoni mwenu wapo watu ambao wamezaliwa wakiwa na sifa na vipaji vya uongozi, lakini uzoefu na tafiti

mbalimbali duniani zinaonyesha kuwa viongozi pia wanajengwa; kwa mafunzo ya masuala mbalimbali ya uongozi, kwa kusoma, kwa kulelewa na kwa kupewa fursa mbalimbali kama hizi. Hivyo basi nataka muelewe mafunzo mliopata ni uwekezaji unaofanywa na Serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo, hivyo basi ili kuhakikisha matumizi mazuri ya rasimali za umma ninaomba mkasome na mkaelimike ili tuone tija na kuwekeza zaidi katika kukuza vipaji vya viongozi. Nimatarajio yangu kuwa mtashiriki kikamilifu katika programu hii ya uongozi na mtakuwa mabalozi wema baadae kwa kushawishi wengine kujifunza.

**Ndugu Washiriki, Wageni Waalikwa, na Wadau Wengine**

Nimefahamishwa moja ya changamoto kuu ni gharama za uendeshaji mafunzo haya iliyopelekea Taasisi ya UONGOZI kuanzisha mfumo wa uchangiaji gharama. Hakika uchangiaji wa gharama ni muhimu sana ili kuhakikisha mafunzo haya yanakuwa endelevu, nawasihi viongozi wa Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Umma na binafsi kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo haya ili viongozi na watumishi waweze kujiunga na mafunzo haya.

Aidha ninaishukuru sana Serikali ya Finland kwa kuwa mdau wetu mkubwa, kwani tangu Taasisi ya UONGOZI inaanzishwa mmekua mkitupatia fedha kwa ajili ya program mbalimbali za Taasisi ikiwemo programu za mafunzo haya. Naomba muendelee kutuunga mkono bila kuchoka ili serikali iweze kufikia malengo yake iliyojiwekea.

Mwisho niwashukuru tena wageni wote kwa kujumuika nasi siku ya leo kushuhudia tukio hili muhimu. Kwa mlio hitimu niwapongeze tena na

kuwatakia utekelezaji mzuri wa yale mlioyasoma. Baada ya kusema hayo, sasa niko tayari kuwatunuku rasmi wahitimu wote vyeti vyenu.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**